OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE

SHULE YA SEKONDARI ILIMA,
S.L.P 546,
TUKUYU.

Simu 0737972805 (Mkuu wa shule) Simu 0764068827 (Makamu Mkuu wa shule)

Tarehe. 07 Desemba 2020

Kumb. Na. RDC/ISS/S.2250/JOIN. INSTR/VOL 1 / 2020.
JINA LA MWANAFUNZI_____
S.L.P _____

_____

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ILIMA WILAYA YA RUNGWE MKOA WA MBEYA MWAKA 2021.

1.0.UTANGULIZI

Ninafuraha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha **KWANZA** katika Shule hii mwaka **2021**. Shule ya sekondari **ILIMA** ipo umbali wa **KM. 12** kusini mwa mji mkuuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe.

Usafiri wa basi kutoka mjini Tukuyu unapatikana katika kituo cha Tukuyu, nauli ni **Tsh 1000/=**

Muhula wa masomo unaanza tarehe **11/01/2021**, unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2020** siku ya jumatatu **Saa 1:00 asubuhi**. Mwisho wa kuripoti ni Tarehe **18/01/2020.**

Mwanafunzi anapaswa kuripoti kwa wakati kwani masomo yataanza toka siku ya kwanza ya kufungua shule.

2.1 SARE ZA SHULE

(a) Wasichana

- Sare ya shule hii ni sketi 2; sketi ya kwanza ni ya rangi ya damu ya mzee na sketi ya pili ni rangi ya blue nyeusi (Dark blue).
- Inatakiwa sketi yenye rinda 16 na ndefu kupita magoti inayogusa kongo 2 za miguu.
- Shati 02 nyeupe tetron mikono mifupi.
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kisigino kifupi vyenye kamba (Gidamu) – Jozi mbili.
- Soksi nyeupe kwa wasichana – Jozi mbili
- Rangi ya hijabu ni nyeupe
- Sare ya michezo kwa shule hii ni Track suit (Dark blue kwa wasichana)
- Raba za michezo rangi nyeusi kwa wasichana
- Vipande vya vitambaa vimeambatanishwa.
- Sare hizi za shule aje nazo zote shuleni siku ya kuripoti tarehe 11/01/2021 ili zikaguliwe.

(b) Wavulana

Sare ya Shule hii ni suruali 2, suruali ya kwanza ni rangi ya damu ya m zee na ya pili ni rangi ya blue nyeusi (Dark blue) inatakiwa suruali pana isiyo bana chini (isiwe modo) yenye rinda mbili mbele kila upande, mfuko mmoja wa nyuma na mikuko 2 juu pembezoni mwa suruali.

- Inatakiwa shati 02 nyeupe zenye mikono mifupi tetron.
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kisigino kifupi vyenye kamba na visivyozidi kwenye kongo mbili za miguu. (isiwe buti)
- Soksi nyeusi kwa wavulana – Jozi mbili
- Sare za michezo kwa shule hii ni Track suit (Dark blue kwa wavulana)
- Raba za michezo rangi nyeusi kwa wavulana
- Vipande vya vitambaa vimeambatanishwa
- Sare hizi za shule aje nazo zote shuleni siku ya kuripoti tarehe 11/01/2021 ili zikaguliwe.

2.2. VIFAA VYA KITAALUMA

Pindi mwanafunzi anaporipoti aje na vifaa vifuatavyo:-

1. Daftari (Counter book 12) Quire 4
2. Kalamu (2- za wino wa blue au nyeusi)
3. Rula ndefu yenye cm 30 moja
4. Mkebe wa hesabu 01
5. Kalamu ya risasi 01 (Pencil)
6. Begi 1 la kubebea madaftari yake.
7. Kamusi moja ya kiingereza kwa kiingereza.

2.3 Chakula cha wanafunzi wa kutwa, nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani pamoja na matibabu anagharamia mzazi / mlezi mwenyewe.

3.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini. Na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti Shuleni

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya Shule kulingana na ratiba ya Shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Prepatation)

d) Kuwahi katika kila shughuli za Shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya Shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika Shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya Shule
g) Hairuhusiwi kuvaa bangili, mikufu, eleni, pete na vipini.
h) Kuvaa sare ya Shule wakati wote unapotakiwa
i) Kuzingatia ratiba ya Shule wakai wote na
j) Kutunza mali za umma.

3.1 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa Shule.

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa y a kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
e) Kupigana na kupiga.
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g) Kudharau Bendera ya Taifa
h) Kuwa mjamzito / kupata mimba
i) Kuoa au kuolewa
j) Kutoa mimba
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa Shule au watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
m) Kuwa na simu ya mkononi

4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa Shuleni na mwanafunzi

a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakapiripoti Shuleni (imeambatanishwa)
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai (imeambatanishwa)
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na Shule

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

Karibu sana Ilima shule ya sekondari.

MWAMBENE J.M
MKUU WA SHULE

HALMASHAURI YA WILAYA RUNGWE.

SHULE YA SEKONDARI ILIMA

A. FOMU YA MZAZI / MLEZI

Mimi..... ambaye ni Mzazi / Mlezi wa Mwanafunzi ..... Ambaye amechaguliwa kujiunga na Elimu ya Sekondari mwaka 2013 shule ya SEKONDARI ILIMA nakubaliana na sheria, kanuni, na maelezo mengine yatakayotolewa na shule.

Sahihi ya Mzazi / Mlezi .....

Tarehe.....Mwaka.....

B. TAARIFA YA MWANAFUNZI

Jina la ukoo.....

Jina la kwanza..... Majina mengine.....

Jinsi..... Tarehe ya kuzaliwa .....

Mahali ulipozaliwa: Kijiji / Mtaa.....Kata..... Wilaya..... Mkoa.....

Namba ya usajili.....

Masomo unayosomea.....

Mwaka wa masomo..... hadi.....

C. AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi..... naahidi kuwa sitashiriki / nitashiriki katika Migomo, Fujo na Makosa ya Jinai katika kipindi chote cha masomo

Tarehe.....Jina.....Sahihi.....

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A:

To the medical Officer, ... From: .....

....

....

..... Date .....

Re: _____

Please Examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time Secondary School studies that may also include military training the Examination should include the following categories (I, iv) each category or Sub – category of which will render the applicant ineligible in case of a defect. Pregnancy (category IV) will also render a girl candidate ineligible for the cause.

I. (a) Eye sight
(b) Hearing
(c) Speech
(d) Limbs
(e) General diseases
(f) Leprosy
(g) Epilepsy

Other serious disease .....
Pregnancy. .....

PART B: MEDICAL OFFICER

(To be completed by a Government medical Officer)

I have Examined the above named and consider that he/she is physically fit for a full time Secondary School studies

(a) Eye - Sight
(b) Hearing
(c) Speech
(e) General diseases
(f) Leprosy
(g) Epilepsy

II. Neuroses .....

III. Other serious diseases .....

IV. Pregnancy .....

DATE: ..... Signature .....

STATION: ..... Date: .....